MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

**Na: 3. Msimu wa Kilimo 2019/20** **Tathmini Oktoba 21-31, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Novemba 1-10, 2019**

**Muhtasari**


- Mvua zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya mazao na malisho.
- Wakulima, wafugaji na wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki.
- Wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika kipindi hiki ikilinganishwa na ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ambayo iliendelea kuimarika. Hali hii ilisababisha kusogea ukanda wima wa mvua maeneo ya kusini hasa katika ukanda wa ziwa Viktoria. Kwa ujumla upepo kutoka kusini mpaka kusini mashariki zilivuma katika maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani lilikuwepo katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi na kusababisha uwepo wa hewa yenye unyevunyevu. Pia migandamizo midogo ya hewa ilitokea baharini kwa kipindi hiki hasa eneo la kaskazini mashariki mwa Madagascar. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kuwa na mchango mdogo kwenye mfumo wa utengenezaji wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Katika dikadi hii vipindi vya mvua za wastani viliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na pwani ya kaskazini. Aidha mvua nyepesi iliripotiwa katika maeneo ya , nyanda za juu kusini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi. Kiasi cha mvua kilichoripotiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi ni kuanzia milimita 26 na zaidi ya milimita 250 kama inavyoonesha katika ramani.




**Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Oktoba 21- 31, 2019.**

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Katika maeneo mengine yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan ukanda wa ziwa Viktoria na nyanda za juu kaskazini mashariki wakulima walijihusisha zaidi nashughuri za upandaji. Kwa maeneo yaliyobaki hususan mkoa wa pwani na Morogoro ya kaskazini wakulima walijihusisha zaidi na uandaaji wa mashamba. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima waliendelea na maandalizi ya mashamba kwa msimu wa kilimo unaotarajiwa kuanza mwezi Novemba hadi Disemba 2019. Wakulima katika mkoa wa Lindi na Mtwara waliendelea na

shughuli za uvunaji wa korosho.Hali ya kuimalika kwa unyevunyevu wa udongo kuliendelea kujitokeza katika maeneo ya pwani ya kaskazini,visiwa vya Zanzibar, ukanda wa ziwa Viktoria na mikoa ya magharibi.Ingawaje upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo umeendelea kupungua katika maeneo ya mkoa wa Simiyu, Shinyanga, Singida , Manyara na Dodoma.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuimalika husussan katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019

Katika kipindi hiki cha dikad, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii itasababisha kuusogeza ukanda wa mvua katika ukanda wa kusini. Hata hivyo katika kipindi hiki kunatarajiwa kuimarika kidogo kwa migandamizo mikubwa iliyopo kusini mwa dunia na kutokea kwa kimbunga Kyarr na migandamizo mengine ya hewa inayotokana na kupanda kwa joto la bahari katika maeneo ya kaskazini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii itapelekea kuchelewesha kwa Ukanda wa mvua kuelekea kusini pia itabadilisha upepo na kuvuma kutoka katika pwani ya nchi yetu na kuelekea baharini hivyo kupunguza uwezekano wa kuwepo mvua katika maeneo mengi. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kuwa na mchango mdogo kwenye mfumo wa utengenezaji wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) kunatarajiwa kupata vipindi vifupi vya mvua katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), Nnyanda za juu Kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) kunatarajiwa kupata hali ya ukavu

## HALI YA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019

Mvua zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya mazao na malisho. Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kwa shughuli za kilimo kama kupanda na kupalilia. Ambako mvua za msimu hajijaanza wakulima wanashauriwa kuendelea kuandaa mashamba.Vilevile wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki.Wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu

.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na utiririkaji wa mito inatarajiwa kuongezeko kidogo katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la ziwa Viktoria. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**
**Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro,** Dar es Salaam-Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***